APRILI 2022

# SHAJARA YA MKUTANO MKUU

**JIWEKE TAYARI!**

Kabla ya kuanza kwa mkutano, unaweza kujiandaa kusikia sauti ya Bwana kwa kutafuta ufunuo wako binafsi.

- ◯ Je, Nimechukua muda kusali sala binafsi?
- ◯ Je, Nimesoma maandiko?

**SEHEMU YA KUANDIKA HAZINA ZAKO MWENYEWE ZA UFUNUO BINAFSI KUTOKA KWENYE MKUTANO MKUU.**

# ULIZA,

Mzee Jeffrey R. Holland alifundisha, “Ufunuo karibu kila wakati huja kujibu swali.”[1]

## NA KISHA SIKILIZA

Mkutano mkuu ni fursa nzuri ya kujifunza kile Bwana angependa ujue na ufanye. Lakini, unajuaje wakati Anazungumza na wewe? Huanza na kufikiria juu ya maisha yako na kile unachohitaji msaada juu yake.

Haya ndio baadhi ya mambo ya kufikiria:

Chukua muda wa kuandika mwongozo wa kibinafsi ambao unatarajia Bwana atakupa wakati wa mkutano.

Unaposikiliza mkutano mkuu, weka maswali haya akilini. Bwana anaweza kukupa mwelekeo wa kibinafsi.






# ANDIKA

Kuna sababu nyingi zinazofanya watu waandike wakati wa mkutano. Kuandika kunaweza kukusaidia kuwa makini zaidi na kukumbuka kile ambacho ulikisikia. Unapoandika, unamwonyesha Bwana kwamba uko tayari kupokea ufunuo binafsi na kuufanyia kazi.

Jaribu! Unaposikiliza mkutano mkuu, usiwe na wasiwasi juu ya kuandika vitu wasemaji wanavyovisema neno kwa neno. Ukikosa kitu, unaweza kurudi na kusoma au kutazama baadaye. Zingatia kuandika mawazo yako na msukumo wakati wa hotuba zao. Ikiwa utaandika kwa wakati huo, hautalazimika kujaribu kukumbuka baadaye.

Kile Walichosema:

Hisia Zangu na Misukumo:

Unahitaji ushauri juu ya jinsi ya kufanya hivyo? Upo hapa:

“Wakati ninapoandika wakati wa mkutano mkuu, siandiki kila ambacho msemaji anasema; ninaandika mwelekeo binafsi ambao Roho hunipatia. Yale*yanayosemwa* si muhimu zaidi ya*tunachosikia* na*tunachohisi*.”

*Mzee Robert D. Hales (1932–2017)*[2]

Kile Walichosema:

**MIALIKO MAALUMU**

Viongozi wa Kanisa mara nyingi wanatupa mialiko ya kutusaidia kukua kiroho. Je, Umesikia mialiko maalum wakati wa vikao? Iandike hapa ili usisahau!



Hisia Zangu na Misukumo:

**SITISHA!**

Je! Umepokea majibu yoyote ya maswali yako hadi sasa? Ikiwa ndivyo, chukua muda kuandika mwongozo na mwelekeo ambao umepokea.

"Naahidi kwamba unapoisikiliza sauti ya Bwana kwako katika mafundisho ya mkutano huu, na kutenda kulingana na msukumo huo, utahisi mkono wa kimbingu juu yako, na maisha yako na ya wale wanaokuzunguka yatabarikiwa."

*Mzee Neil L. Andersen*[3]

Baraka kuu za mkutano mkuu zinatujia baada ya mkutano kumalizika. Kumbuka mfano uliorekodiwa mara kwa mara katika maandiko: tunakusanyika kusikia maneno ya Bwana, na tunarudi majumbani kwetu kuyaishi.

*Mzee Robert D. Hales*[4]

Kile Walichosema:

Hisia Zangu na Misukumo:

**SITISHA!**

Je! Umepokea maoni zaidi juu ya vitu unavyohitaji kuendelea kufanya, kuacha kufanya, au kuanza kufanya ili kuboresha maisha yako?

**MIALIKO MAALUMU**

Viongozi wa Kanisa mara nyingi wanatupa mialiko ya kutusaidia kukua kiroho. Je! Umesikia mialiko maalum wakati wa vikao? Iandike hapa ili usisahau!



# NI NINI KINACHOFUATA KWANGU?

Umekuwa ni uzoefu mzuri kiasi gani kusikiliza shuhuda za mitume na manabii! Je, Ulipokea mwelekeo ambao unaweza kukusaidia katika maisha yako?

Sasa ni wakati mzuri wa kuweka malengo ya kukusaidia kutenda juu ya mambo ambayo umejifunza. Hapa ni baadhi ya mawazo:

- ◯ Chagua sehemu moja au mbili za mwelekeo wa kibinafsi na uunde mpango wa kutenda.
- ◯ Fanya mpango wa kufanyia kazi moja ya changamoto au mialiko uliyosikia.
- ◯ Sikiliza hotuba ya mkutano kila asubuhi wakati unajiandaa kwenda shule.
- ◯ Shiriki moja ya hadithi zako au nukuu pendwa kutoka katika mkutano mkuu na rafiki au kwenye mitandao ya kijamii.
- ◯ Panga wakati ambapo familia yako inaweza kushiriki kile kilichowapendeza kila mmoja wao wakati wa mkutano mkuu.
- ◯ Je! Una wazo lingine? Andika lengo lako mwenyewe:

____________________

____________________

____________________

____________________

Tumia mkasi kukata sehemu hii ya ukurasa huu. Kisha unaweza kuiweka mahali utakapoweza kuona kila siku kukukumbusha malengo yako!

“Majibu ya sala zako maalum yanaweza kutoka moja kwa moja kutoka kwenye hotuba fulani au kutoka kwenye kifungu fulani. . . . Nia ya dhati ya kusikia na kufuata maneno ya ushauri itatayarisha njia ya ufunuo binafsi.

*Mzee Dieter F. Uchtdorf*[5]

**JE, UNAHITAJI NAKALA ZAIDI?**

Pakua na uchapishe shajara hii kwenye **conference.ChurchofJesusChrist.org.**


**Muhtasari**

1. Jeffrey R. Holland, “Cast Not Away Therefore Your Confidence,” *Ensign*, Machi 2000, 9.
2. Robert D. Hales, mkutano mkuu wa Oktoba 2013 (*Ensign,* au *Liahona,*, Novemba 2013, 6).
3. Neil L. Andersen, mkutano mkuu wa Okt. 2017 (*Ensign* au *Liahona,*, Nov. 2017, 126).
4. Robert D. Hales, mkutano mkuu wa Oktoba 2013 (*Ensign* au *Liahona*, Novemba 2013, 7).
5. Dieter F. Uchtdorf, “Mkutano Mkuu—Hakuna Baraka za Kawaida,” *Ensign* or *Liahona*, Sept. 2011, 4.



© 2022 na Intellectual Reserve, Inc.
Haki zote zimehifadhiwa.

IDHINI YA KUCHAPISHA UPYA KIJITABU HIKI IMETOLEWA KWA MATUMIZI BINAFSI, YASIYO YA KIBIASHARA. HII INAJUMUISHA IDHINI KWA VIONGOZI WA KATA KUCHAPISHA IDADI NDOGO YA NAKALA KWA AJILI YA WALE WANAOWAHUDUMIA KWA KIGEZO CHA MIITO YAO. VIJITABU SHARTI VICHAPISHWE KWA UKAMILIFU WAKE. HII HAIJUMUISHI IDHINI YA KUCHAPISHA MTANDAONI, KUTUMIA TENA AU KUSAMBAZA NYENZO HII. MATUMIZI YOYOTE YA ZIADA YA NYENZO HII YANAHITAJI KUIDHINISHWA.

**permissions.
ChurchofJesusChrist.org**



KANISA LA
YESU KRISTO
LA WATAKATIFU
WA SIKU ZA MWISHO